Uhasama wa Nyumbani na Watoto

JAMII SALAMA KWA WATOTO

Kila uhusiano una panda shuka zake.
Dhiki na mabishano katika familia ni kawaida.

Walakini, ikiwa mabishano yatakuwa mbaya zaidi na kuna mgongano, hofu, udhibiti na vitisho hii inamaanisha kuna shida na sio kawaida tena!

Hii inaitwa Uhasama wa Nyumbani.

Aina za uhasama wa nyumbani zinaweza kuwa:

- **Kimwili** — Kusukuma, kutikisa, kuchapa kofi, kukulazimisha kufanya mambo ya kingono, kukurushia vitu, kuharibu mali yako.
- **Kihemko** — Kukutisha, kuzungumza kwa njia inayoogopesha, kukuweka chini.
- **Kichumi** — Kudhibiti pesa zako, kukufanya uombee pesa bila kufikiria.
- **Kijamii** — Kukutukana mbele ya watu wengine, kukutenga na familia yako na marafiki, kudhibiti unachofanya na unapoenda.
- **Kiroho** — Kutokuruhusu kuwa na maoni yako mwenyewe kuhusu dini, utamaduni, mila na desturi.

Ikiwa wewe ndiye mtu anayeadhirika, kimwili na/au kihemko, kuna sheria na mipango ambayo itakusaidia kujikinga wewe na watoto wako. Kuna mipango pia inayopatikana kwa watu ambao wanaotusi wewe na watoto wako, ili kuwasaidia kuacha.

Uhasama dhidi ya mwenzi au watoto ni mbaya na ni kinyume cha sheria.

Uhasama wa nyumbani hutisha watoto na unaweza kuwadhuru. Wakati mwingine wazazi hufikiri watoto hawasikii au hawajui mambo mabaya yanayofanyika nyumbani lakini watoto hujua.

Watoto wote ambao hupitia uhasama wa nyumbani huathiriwa nao kwa njia kadhaa, kimwili na/au kihemko.

Vidonda vya kihemko za uhasama wa nyumbani mara nyingi hudumu maisha yote.

Watoto, ambao wameshuhudia uhasama wa nyumbani, wanaweza kuwa na shida za kusoma, kulala, kukojoa kitandani,

kusikizana na watoto wengine au kuonekana kutengwa.

Ni wajibu wako kulinda watoto wako kutokana na athari za uhasama wa nyumbani.

Kama mzazi wewe ndiye mtu wa muhimu kabisa katika maisha ya mtoto wako na wanajifunza kutoka kwako. Watoto wanaokua katika nyumba yenye uhasama hujifunza kutatua matatizo kutumia uhasama.

Wakati uko katika uhusiano wenye uhasama unahitaji kujilinda.

Unastahili bora.

Wakati mwingine ni vigumu kutatua matatizo ya familia peke yako. Ni sawa kuomba msaada. Kuna mashirika ambayo yanaweza kukusaidia. Hata ikiwa ulijaribu hapo awali, jaribu tena kupata msaada ambao unafaa kwako.

Wakati uko katika uhusiano wenye uhasama ni vigumu kulinda watoto wako.

Zungumza na mtu unayeamini kuhusu kinachotendeka kwa watoto wako. Wanaweza kuwa hawako SAWA. Zungumza na daktari wako, mwalimu wao au mtunzaji wao wa mtoto, mfanyikazi wa kesi au rafiki. Waulize unaweza kupata msaada wapi ikiwa unafikiria wanauhitaji.

Ikiwa utampiga mwenzako, jaribu kumdhibiti au kumtisha, unahitaji kuacha.

Ni kinyume cha sheria. Zungumza na mfanyikazi wako wa kesi, mshauri, kiongozi wa jamii, mchungaji au mtu unayeamini kuhusu unachofanya.

Kuna mipango ya kukusaidia kuacha tabia ya uhasama na kudhibiti hasira yako.

Ikiwa watoto wako wanaumizwa kimwili au kihemko na uhasama wa nyumbani, basi serikali inaweza kuhusika na familia yako.

Familia kutoka kwa asili za wakimbizi zinaweza kuchanganyikiwa kwanini serikali inashughulika na maswala yao ya familia. Walakini, sheria inasema kwamba Usalama wa Mtoto lazima ihusike wakati inapokea simu ya hoja kwamba mtoto anaweza kuwa ameadhiriwa.

Watoto hujifunza kutoka kwa wazazi wao na ni muhimu kwako kuonyesha mifano mizuri kwao.

Wanahitaji mtu mzima katika maisha yao ambaye anapenda na kusaidia.

Wanahitaji pia nyumba ya salama ili kukua watu wazima wenye afya na furaha.

Watoto wote wanastahili utoto salama, wenye afya na furaha.

Ikiwa uko katika hatari ya mara moja piga simu 000 kila mara.

Hapa kuna orodha ya baadhi ya mashirika ambayo yanaweza kukusaida:

- **Huduma ya Mtafsiri wa Simu (TIS) Simu ya Kitaifa**
  131 450 (masaa 24 kwa siku, siku 7).
- **Dvconnect Laini yaWanawake**
  1800 811 811 (masaa 24, siku 7)
  Laini ya simu kwa wanawake na watoto wanaopitia uhasama wa nyumbani
- **Dvconnect Laini ya Wanaume**
  1800 600 636 (9am – midnight, yaani saa tatu asubuhi mpaka saa sita usiku, siku 7)
  Huduma ya ushauri wa simu kwa wanaume kuhusu uhasama wa nyumbani na familia, matatizo ya uhusiano.
- **Kituo cha Utunzaji wa Kipeo QLD**
  1800 177 135 (masaa 24)
  Huduma ya jimbo zima ya ushauri wa simu na matatizo.
- **Huduma ya Msaada wa Wanawake Wahamiaji (IWSS)**
  (07) 3846 5400 (Mpango wa shambulio ya kingono)
  (07) 3846 3490 (Mpango wa uhasama wa nyumbani)
  Shirika la msingi wa jamii wa matatizo na msaada ambao hufanya kazi na wanawake na watoto wasiozungumza Kiingereza.
- **Kinections**
  (07) 3435 4300
  Shirika la msingi wa jamii linalopeana ushauri kwa watu wa asili ya wasiozungumza Kiingereza.
- **Lifeline**
  13 1114
  Ushauri wa simu, habari na huduma ya kurejea inapatikana masaa 24 kwa siku.
- **Laini ya Wanaume Australia**
  1300 78 99 78
  Ushauri wa simu masaa 24 na huduma ya kurejea kwa wanaume.
- **Uhusiano Australia**
  1300 364 277
  Huduma za ushauri wa uhusiano kote Queensland.
- **Msaada wa Kisheria Queensland**
  1300 65 11 88
  Hutoa habari ya bure ya kisheria, ushauri na uwakili.
- **Huduma za Kisheria za Wanawake**
  (07) 3392 0670 / 1800 677 278
  Kituo cha kisheria cha jamii kwa wanawake. Wanafafanua sheria na kinachotendeka kortini kwa maswala mengi ya kisheria. Hawafanyi uwakili wa korti lakini watatoa ushauri kuhusu haki za kisheria na habari.

MDA Multicultural Development Association

This document was developed by Multicultural Development Association (MDA) with funding from the Australian Government Department of Families, Housing, Community Services and Indigenous Affairs (FaHCSIA)